# SIKU 100



## ZA MHE. RAIS SAMIA


**WIZARA YA NISHATI**



# UTEKELEZAJI WA AHADI ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, NDANI YA SIKU 100 ZA SERIKALI

Utekelezaji wa ahadi na maelekezo ya Mhe. Rais kwa Wizara ya Nishati katika kipindi cha siku 100 za uongozi wake hususan katika matumizi ya nishati safi ya kupikia, usambazaji wa umeme, mafuta pamoja na Gesi.





# NISHATI SAFI YA KUPIKIA

Kugawa majiko banifu 13,575 kwa ruzuku ya asilimia 85 pamoja na majiko janja ya umeme (induction cookers) 7,292. Usambazaji wa majiko haya umefanya Idadi ya watumia wa Nishati kuongezeka hadi kufikia 23%.





Kugawa mitungi ya gesi ya LPG 27,153 ya kilo sita (6) kwa ruzuku ya asilimia 50. Mitungu hii inapatikana kwa Mawakala wa Gesi katika Wilaya zote 139 nchini.

Taasisi 22 zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku zimehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia katika kipindi cha siku 100, hivyo kufikisha jumla ya taasisi 1,069 zinazotumia nishati safi.





Kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Pwani ambapo nyumba 470 na shule moja zimeunganishwa mkoani Lindi, na nyumba 530 zimeunganishwa mkoani Pwani.

Kutoa mafunzo kuhusu Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa maafisa 116 ambao ni waratibu wa nishati safi ya kupikia ngazi ya mikoa na halmashauri.





Ujenzi wa mitambo miwili ya kuzalisha mkaa mbadala katika Mikoa ya Dodoma na Tabora ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza Februari, 2026.



# KUSAMBAZA UMEME

Kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa kupeleka Umeme katika Vitongoji 9,009 wenye thamani ya shilingi Trilioni 1.2. Mikataba 30 imesainiwa na kati ya hiyo Mikataba 21 ni ya Kampuni za Wazawa.Mradi huu ukikamilika utanufaisha wateja wa awali 290,300 katika mikoa 26 ya Tanzania bara.





Miradi 235 ya kusambaza umeme kupitia TANESCO imetekelezwa na kuwezesha kuunganishwa kwa wateja wapya 210,997.

Jumla ya vitongoji 39,888 kati ya 64,359 sawa na asilimia 62 tayari vimeunganishwa na umeme.






Ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha nguzo za zege kinachomilikiwa na TANESCO mkoani Tabora chenye uwezo wa kuzalisha nguzo 100 kwa siku umekamilika. Uzalishaji wa nguzo hizi utasaidia katika kuunganisha wateja wapya takribani milioni 1.7 kwa mwaka.

Uzinduzi wa matumizi ya Mita Janja za Umeme (Smart Meters), ambapo hadi sasa mita 47,341 zimefungwa kwa wateja mbalimbali nchini na zoezi linaendelea.





Uzinduzi wa Mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera kwa kukiongezea nguvu kituo hicho kwa kufunga transfoma mbili ambapo kila moja ina uwezo wa MVA 10. Kukamilika kwa mradi huu kumetatua changamoto ya upotevu mkubwa wa umeme na huduma isiyo ya uhakika kwa wilaya za Mpwapwa, Kongwa na Kilolo (Ismani), ambazo hapo awali zilitegemea umeme kutoka umbali wa zaidi ya kilomita 155.




# NISHATI VIJIJINI




Wizara ya Nishati imeanza mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Nishati Vijijini Na. 8 ya mwaka 2005 lengo likiwa kupanua wigo wa Mfuko wa Nishati Vijijini (REF) kuhudumia na maeneo ya mijini katika masuala ya nishati safi ya kupikia.

# MAFUTA NA GESI



Ujenzi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) unaendelea vizuri na kwa sasa umefikia asilimia 78.8 ya utekelezaji, ambapo kilomita 521 kati ya 1,443 tayari zimeunganishwa na kufukiwa ardhini.

Mradi wa Bomba la Mafuta umewezesha ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa Kampuni 2,000 za Kitanzania zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.325.


Ajira 9,194 zimetolewa kupitia mradi wa bomba la mafuta huku wananchi 170 wakiwa wamepatiwa mafunzo maalum ya kufikia viwango vya Kimataifa katika ujenzi wa miradi ya mafuta na gesi.



Uchimbaji huu wa Gesi asilia katika Kitalu cha Mnazi Bay unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa Gesi Asilia kwa kiasi cha Futi za Ujazo milioni 51 – 134 kwa siku (mmscf) wakati Kitalu cha Ntorya kinatarajiwa kuongeza uzalishaji kwa futi za ujazo milioni 60 kwa siku (mmscf) na hivyo kuleta manufaa kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.



Serikali imeendelea kusimamia uagizaji, uhifadhi na usambazaji wa mafuta nchini, ambapo uwezo wa kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Mtwara umeongezeka kutoka tani 29,280 hadi tani 110,221.




Mradi wa ujenzi wa ghala kubwa la kuhifadhi mafuta (Single Receiving Terminal) katika Bandari ya Dar es Salaam unaendelea vizuri na kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 30, likiwa na uwezo wa kuhifadhi tani 308,110.




TPDC inakamilisha taratibu za ununuzi wa vituo vitano vya CNG vinavyohamishika kwa ajili ya kuongeza matumizi ya gesi asilia nchini.




Serikali imetoa vibali vya ujenzi wa vituo vinne vya CNG (Compressed Natural Gas), vibali vitano vya usafirishaji wa gesi asilia kwa mabomba pamoja na leseni za kujazia na kusambaza CNG.



Mpaka sasa jumla ya magari na bajaji 16,154 yanatumia gesi asilia ya (CNG).



Serikali kupitia TPDC inaendelea kushirikiana na Kampuni ya ARA Petroleum Tanzania Limited katika maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Ntorya hadi Madimba mkoani Mtwara.



Serikali imekamilisha maandalizi ya kuchimba visima vipya vinne vya gesi asilia; vitatu katika Kitalu cha Mnazi Bay mkoani Mtwara na katika eneo la Ntorya, Kitalu cha Ruvuma.




# HITIMISHO

Mafanikio haya ni ushahidi tosha wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inyoongozwa na Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya uhakika, nafuu na endelevu kwa maendeleo ya Taifa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA NISHATI**

# VIONGOZI WAKUU



**Mhe. Deogratius John Ndejembi**

Waziri wa Nishati



**Mhe. Salome Wycliffe Makamba**

Naibu Waziri wa Nishati



**Mha. Felchesmi Mramba**

Katibu Mkuu - Umeme na Nishati Jadidifu



**Dr. James Peter Mataragio**

Katibu Mkuu - Mafuta na Gesi Asilia